**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**686** **VITENDO VYA KUJIFUNZA KISWAHILI**

**Muda: Saa 3.** **Jumatatu, 06 Mei 2013**

---

**MAELEKEZO.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu **B** and **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **40** na sehemu **B** na **C** zina alama **30** kila moja.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Tofautisha kati ya "matamshi" na "tamko" katika muktadha wa ufundishaji wa lugha.
2. Fafanua kwa kifupi umuhimu wa mwalimu kuiga sauti za wanyama na vitu ili kufundisha fonimu.
3. Ainisha hatua nne za kufundisha maneno mapya kwa kutumia kadi za maneno
4. Eleza jinsi utumiaji wa nyimbo na mashairi unavyoweza kusaidia mtoto mwenye aibu kujifunza lugha. (Hoja nne).
5. Taja sababu nne zinazoweza kufanya mtoto asishiriki kikamilifu katika mazungumzo darasani.
6. Fafanua kwa kifupi mambo manne ambayo mzazi anaweza kufanya ili kukuza stadi ya kusoma kwa mtoto akiwa nyumbani.
7. Bainisha manufaa manne ya kumtumia mwanafunzi bora kumsaidia mwenzake katika ujifunzaji wa lugha.
8. Eleza kwa kifupi dhana ya "mahusiano ya herufi na sauti" na kwa nini ni muhimu. (Mambo mawili).
9. Ainisha mazoezi manne ya mikono yanayomwandaa mtoto kwa stadi ya kuandika.
10. Kwa kutumia mfano, fafanua kwa kifupi jinsi mwalimu anavyoweza kutumia mchezo wa "Nani Anazungumza" kufundisha stadi ya kusikiliza.

**SEHEMU B (Alama 30)**

Jibu maswali mawili (2) kutoka sehemu hii.

11. "Ukosefu wa lugha sanifu katika familia unaweza kusababisha changamoto kubwa kwa mtoto anayeanza shule." Jadili kauli hii kwa hoja tano.
12. Fafanua kwa kina jinsi utakavyotumia mbinu ya mzunguko wa hadithi kukuza stadi za usimulizi na mawasiliano. (Hoja tano).


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

13. Chambua mambo matano ambayo mwalimu anapaswa kuzingatia anapobuni vitabu vya hadithi vya picha kwa ajili ya darasa lake.

**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali mawili (2) kutoka sehemu hii.

14. Eleza hatua tano za kufundisha watoto jinsi ya kuunda sentensi rahisi, na kisha jinsi ya kuziandika kwa usahihi.

15. "Mwalimu ni mchezaji, mwanamuziki na msimulizi." Fafanua jinsi mwalimu anavyoweza kutumia vipaji hivi vitatu kufundisha stadi za lugha kwa ufanisi. (Hoja tano).

16. Bainisha mikakati mitano utakayoitumia kumsaidia mtoto anayekosea kuunganisha sauti za herufi kuwa neno (k.m. anasema /m/ /a/ /m/ /a/ lakini anashindwa kusema 'mama').


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org